

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



1 JUNI, 2021



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA AROBAINI NA MOJA – TAREHE 1 JUNI, 2021

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA NISHATI:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nishati kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa

majukumu ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

III. MASWALI:

OFISI YA WAZIRI MKUU:

341. **MHESHIMIWA DKT. THEA MEDARD NTARA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Je, ni lini Serikali itaboresha Sheria ya Ajira na kuweka mazingira mazuri ili Maprofesa wa kigeni waweze kufanya kazi nchini.

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

342. **MHESHIMIWA DAVID MWAKIPOSA KIHENZILE (MUFINDI KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itapeleka Gari la Wagonjwa katika Kituo cha Afya cha Mgololo.

343. MHESHIMIWA EMMANUEL ADAMSON MWAKASAKA (TABORA MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kukarabati barabara zilizoharibika hasa barabara za Vijijini.

344. MHESHIMIWA DAUD PROTAS VENANT (IGALULA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Barabara ya Igunga – Miswaki – Loya – Migongwa – Maguliati hadi Iyumbu Singida yenye urefu wa Km 89.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

345. MHESHIMIWA MARGARET SIMWANZA SITTA (URAMBO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, Serikali inachukua hatua gani katika kutatua mgogoro wa Mipaka kati ya Jeshi la


Magereza na Wananchi wa Kata ya Ukondamoyo hususan Kijiji cha Tumaini Wilayani Urambo.

WIZARA YA MAJI:

346. MHESHIMIWA KASALALI EMMANUEL MAGENI (SUMVE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kupeleka Maji ya Ziwa Victoria katika Jimbo la Sumve.



347. MHESHIMIWA ALOYCE JOHN KAMAMBA (BUYUNGU):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

- (a) Je, ni kwanini Miradi ya Maji katika Mji wa Kakonko haijakamilika kwa muda mrefu;
- (b) Je, ni lini Mji wa Kakonko na Vitongoji vyake utapata maji safi, salama na ya kutosha.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,
JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**348. MHESHIMIWA JAPHET NGAILONGA
HASUNGA (VWAWA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya,
Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na
Watoto:-

Je, ni lini Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa
Songwe itakamilika na kuanza kutoa huduma
kwa Wananchi wa Mkoa wa Songwe.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

**349. MHESHIMIWA ANASTAZIA JAMES
WAMBURA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na
Uchukuzi:-

- (a) Je, ni nini sababu ya Barabara ya Kibiti –
Lindi kuharibika mara kwa mara licha ya
kufanyiwa ukarabati;
- (b) Je, Serikali ina mpango gani wa kutatua
tatizo hilo ili kuzuia ajali za mara kwa mara
katika barabara hiyo.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

350. MHESHIMIWA JERRY WILLIAM SILAA (UKONGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-

- (a) Je, ni Taasisi ngapi zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango hadi sasa hazina Bodi au Bodi zake zimemaliza muda wake;
- (b) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuanzisha Benki ya waliopekuliwa ili muda wowote uteuzi ufanyike haraka kusaidia Taasisi hizo kwenda na kasi ya Serikali kwani kwa sasa upekuzi umekuwa ni kisingizio cha kuchelewesha uteuzi.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**DODOMA
1 JUNI, 2021**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**